BARAZA LA HABARI TANZANIA

Nyumba No. KUN/MTN/532, Barabara ya Bagamoyo, Tegeta Skanska,
S. L. P 10160, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu:+255 719 494640 / 767 494826
Barua pepe: media@mct.or.tz
Tovuti: http://www.mct.or.tz
S.L.P 3490, Zanzibar

House No. KUN/MTN/532, Bagamoyo Road, Tegeta Skanska Area,
P.O.Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 719 494640 / 767 494826
Email: media@mct.or.tz
Website: http://www.mct.or.tz
P.O.Box 3490, Zanzibar

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## Vyombo vya habari viache kukiuka maadili

Septemba 08, 2025

**Dar es Salaam:** Baraza la Habari Tanzania (MCT) linatoa wito kwa vyombo vya habari, waandishi wa habari na watangazaji nchini kuzingatia kwa dhati maadili ya taaluma ya habari kama yalivyoainishwa katika miongozo na kanuni za Baraza. Wito huu unakuja kufuatia matukio ya hivi karibuni yanayoashiria ukiukwaji wa maadili, hususan katika utoaji wa taarifa zisizo sahihi, zenye kuchochea au kukosa uwiano wa kitaaluma.

Kanuni za maadili toleo la 2020 kuhusu maadili ya uandishi wa Habari kipengele cha 7; kinasisitiza haki ya kujibu kwa wale wanaotuhumiwa au kuhusishwa katika habari.: *"Waandishi wa habari watatoa fursa na haki ya kujibu waliohusika au taasisi/mashirika iliyoathiriwa au kuhusishwa kwenye habari kabla ya kuchapisha au kutangaza habari husika. Habari itaendelea tu bila ya majibu iwapo mhariri amejiridhisha kwa ukamilifu kuwa hatua zote muhimu zimezingatiwa.*

Aidha, Kanuni hizo zinasisitiza kuwa, "*Pale ambapo mhariri ana ushahidi wa kutosha kuwa hana shaka ya ukweli au usahihi na uhakika wa jibu au ufafanuzi atakuwa na uhuru wa kuongeza maelezo machache mwisho wa ufafanuzi kuonyesha msimamo wake kuhusiana na suala hilo."*

*"Maneno yana maana. Picha zina maana, na namna tunavyoeleza habari zetu kwa umma ina maana kwa sababu inaweza kutuunganisha au kutugawa. Uandishi wa habari wenye uwajibikaji ni ule unaoepuka uchochezi, unaokataa lugha ya chuki na kutoa nafasi sawa kwa pande zote,"* inasema sehemu ya kanuni za maadili toleo la 2020 la MCT.

Kwa kutambua changamoto za kisasa kama vile kusambaa kwa taarifa potofu (misinformation), taarifa za uongo (disinformation), na hotuba za chuki (hate speech), Baraza la Habari mwaka huu limekwishatoa mafunzo kwa wahariri, watangazaji na waandishi wa habari katika mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Visiwani

Zanzibar. Mafunzo haya yanalenga kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuwa makini, waadilifu na wenye weledi katika kazi zao, hususan katika mwaka huu wa uchaguzi.

Hata hivyo, ufuatiliaji wa  mwenendo wa vyombo vya habari umebaini bado baadhi ya vyombo vya habari vikiwemo vya mtandaoni bado vinakiuka maadili na kutozingatia kuchapisha au kutangaza taarifa zisizo sahihi na kutozingatia misingi ya kumpatia mtuhumiwa haki ya kujibu.

MCT inasisitiza kuwa kufuata maadili ni wajibu wa kitaaluma; na hiyo ndiyo kinga kwa waandishi wa habari dhidi ya hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa na mamlaka husika dhidi yao..

MCT inahimiza vyombo vyote vya habari kuwa walinzi wa ukweli, ambao ndio silaha kubwa katika zama hizi za taarifa nyingi na upotoshaji wa haraka. Ni jukumu la kila chombo cha habari kuhakikisha kuwa taarifa inayoifikia jamii imechunguzwa, imehakikiwa na inaakisi ukweli..

Baraza la Habari Tanzania, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1995 na wadau wa habari, limekuwa nguzo ya kujisimamia kitaaluma kwa wanahabari nchini. Kupitia miongozo na kanuni zinazokubalika na kuheshimiwa na wanachama wake, MCT linaendelea kusimamia maadili, kuhimiza weledi na kulinda hadhi ya taaluma ya habari.

*Ernest S. Sungura*
**Katibu Mtendaji**